*SWAHILI FORUM 30 (2023): 117-137*

# KISWAHILI KATIKA ENZI YA UTANDAWAZI: BAINA YA AFRIKA NA AMERIKA

ALAMIN MAZRUI NA KIMANI NJOGU

The rise of Swahili in the American academy in the 1960s was prompted by two forces: African identity politics among African Americans, on the one hand, and the politics of the Cold War between the USA and the Soviet Union, on the other. Both these sources of Swahili ascendency were themselves a response to the unfolding dynamics and counter-dynamics of independence politics in “Swahiliphone” Africa, that is in the East African nations where the Swahili language was in wide use. But now that the Cold War is over more or less, and the nature of African American politics has undergone significant change in focus, what is the fate and direction of Swahili studies in the USA? This is the central question that this article will seek to address as it considers, at the same time, the shifting disciplinary areas with which the study of Swahili has been associated. In the process the article will also touch on the state of Swahili studies in some other spaces of the world.

## Kitangulizi

Enzi ya utandawazi si enzi iliyoanza juzi na jana; ni enzi iliyojitokeza kwa njia mbalimbali katika sehemu mbalimbali za dunia kwa karne nyingi. Hatuna budi kukubaliana na Manfred Steger kuwa “*Globalization is not a single process but a matrix of processes that operate simultaneously and unevenly in different forms across all geographical scales and across many dimensions*” (2020: 36–37), yaani “Utandawazi si mkondo wa aina moja bali ni mkusanyiko wa mikondo mingi inayokwenda pamoja pasi na kuwa sambamba katika hali mbalimbali na inayokata sehemu zote za kijiografia na nyanja nyingi nyingine.” Historia yake ni ndefu ingawa kasi yake imeongezeka sana katika hii miongo ya karibuni kutokana na maendeleo makubwa yaliyotokea katika teknolojia za usafiri, za habari, na za mawasiliano. Lakini katika makala hii, lengo letu ni kuyazingatia “masomo ya Kiswahili” katika muda wa utandawazi wa hii miaka sitini tu iliyopita – kuanzia miaka ya 1960 mpaka leo.

Pia tunadhamiria kuitazama mada hii kwa kuangalia uhusiano wa Kiswahili na “Uswahili” si na dunia nzima, bali na nchi ya Amerika tu. Amerika ndilo taifa ambalo sote wawili tunalifahamu zaidi – tumesomea hapo, na Alamin Mazrui ameendelea kufanya kazi hapo tangu 1990. Lakini sababu kubwa zaidi ya kuifanya Amerika kitovu cha uchambuzi wetu ni ile nafasi yake kubwa katika bahari ya utandawazi – kiuchumi, kiutamaduni n.k. Hakuna nchi nyingine yenye mtambo wenye nguvu zaidi wa kusukumia utandawazi duniani kama Amerika, hasa kuanzia miaka ya 1960. Ingawa katika kipindi cha uraisi wa Donald Trump na mwito wake wa “*America First*” (Amerika Kwanza), Amerika ilionekana kutaka kujitenga na baki ya ulimwengu, ukweli ni kwamba nguvu zake ziliendelea kuathiri mwelekeo wa utandawazi kiuchumi na kwa njia nyenginezo. Hata kuna

wale wanaoitakidi kwamba mpaka leo hakuna tofauti kubwa baina ya utandawazi na hali ya "kuamerikika" kitamaduni.

Tunafahamu kwamba "masomo ya Kiswahili" ni dhana ambayo inaweza kuwa na maana mbalimbali katika hali mbalimbali za matumizi yake. Inajumuisha fani mbalimbali zinazokusudiwa kutafiti hali mbalimbali za "Uswahili" – lugha, utamaduni, historia, sanaa, falsafa na kadhalika – kwa mtazamo wa kimataifa. Lakini kwa muktadha wa nchi ya Amerika, masomo ya Kiswahili hayajakuwa na maana zaidi ya mafunzo ya lugha yenyewe ya Kiswahili. Ingawa baadhi ya vyuo hufundisha kazi za fasihi na utamaduni, lengo kubwa huwa ni kukitilia nguvu Kiswahili ambacho wanafunzi wa lugha hiyo wameweza kukimudu. Lakini tutaona kwamba kuna tofauti kubwa za madhumuni – ikiwa ni ya dola, ya jumuiya, au ya mtu binafsi -- ya kufundisha na kujifunza lugha yenyewe. Kwa hivyo, ingawa hatuiingilii mada ya "Critical Swahili Studies" (Masomo Chambulizi ya Kiswahili) waziwazi, makala yetu yadhihirisha kwamba mara nyingi ufundishaji na ujifunzaji wa lugha hii nchini Amerika huwa ni vitendo vya kisiasa.

Kwa kiasi kikubwa ufundishaji wa masomo ya Kiswahii katika baadhi ya vyuo vya Uzunguni – Uingereza, Ujerumani, Ufaransa, – ulitokana na historia ya ukoloni. Lakini, ingawa huenda kulikuwa na vyuo viwili vitatu vilivyosomesha Kiswahili tangu siku za ukoloni, ufundishaji wa Kiswahili katika vyuo vingi vya Amerika ulitokea katika kipindi cha historia ya Afrika baada ya ukoloni. Na yaliyosababisha masomo ya Kiswahili kupata nguvu katika vyuo vya Amerika katika wakati huu wa miaka ya 1960 ni mambo mawili: (1) Mwamko wa siasa za nasaba miongoni mwa Waamerika wa asili ya kiAfrika (African Americans), na (2) Siasa za Vita Baridi (Cold War). Mambo mawili haya yanadhihirisha mgongano baina ya mikondo miwili mbalimbali ya utandawazi – mkondo wa utandawazi uliofungamana na harakati za ukombozi, kwa upande mmoja, na mkondo wa utandawazi unaoendeleza siasa za utawala wa kikoloni na ukoloni mamboleo, kwa upande mwingine. Lakini shina la sababu zote hizi mbili zilizokipa Kiswahili msukumo mkubwa katika vyuo vya Amerika ni matukio ya kisiasa yaliyotokea katika nchi za Afrika Mashariki. Hebu sasa tuangalie kwa undani kidogo namna gani siasa za Afrika Mashariki zilivyokuja kuathiri usomeshaji wa Kiswahili nchini Amerika katika kipindi hiki cha miaka ya 1960.

## Kiswahili, Umajumui wa Afrika na Mvumuko wa Watu Weusi

Kama tujuavyo, kwa karne nyingi Waamerika wa asili ya kiAfrika walikuwa wamefanywa waionee aibu asili yao ya kiAfrika. Waamerika wengine wote walikuwa wakijulikana kwa asili zao – Italian American, German American, Irish American n.k. Lakini kitu kilichotiliwa mkazo katika utambulishaji wa Waamerika wa asili ya kiAfrika siku zote kilikuwa ni rangi yao tu – wakiitwa waNegro, na baadaye Blacks (Weusi)! Waamerika wengine wote wakapewa sababu ya kitamaduni

ya kujivunia kule walikotoka wahenga wao; lakini Waamerika wa asili ya kiAfrika walifanywa wajihisi kwamba kujinasibisha na Afrika ni kama kujipaka uchafu!

Hali hii ilianza kubadilika taratibu taratibu, kwanza kutokana na kuibuka kwa Umajumui wa Afrika (Pan-Africanism), dhana iliyochimbukana hasa na fikra za watu kama Martin R. Delaney (1812-1885), Alexander Crummell (1822-1898), na Edward Wilmot Blyden (1832-1912). Kuanzia 1937, Paul Robeson (1898-1976) na chama chake cha Baraza la Masuala ya Afrika (Council on African Affairs) walifanya kazi kubwa ya kuisambaza dhana hii ya Umajumui wa Afrika miongoni mwa Waamerika wa asili ya kiAfrika. Baadaye, kama tujuavyo, viongozi wa kwanza wa Afrika huru, viongozi kama Kwame Nkrumah na Jomo Kenyatta, walikuwa pamoja na wenzao wa kutoka Amerika na Caribbean – kina W. E. B. Du Bois, George Padmore, Ras MacKonnen na wengineo – katika harakati za Umajumui wa Afrika kule Ulaya. Na hatimaye hii dhana ya Umajumui wa Afrika ilikuja kukipa Kiswahili mvuto fulani si miongoni mwa Waamerika wa asili ya kiAfrika tu, lakini pia miongoni mwa Waafrika wa nchi nyingine za Afrika, kama Ghana, Nigeria, na Misri.

Kama jina lake linavyodhihirisha, Umajumui wa Afrika ulikuwa umekusudia kuwaunganisha watu wote wa asili ya kiAfrika duniani. Katika hali ya nadharia za ugozi za wakati ule, neno “uafrika” na neno “weusi” yalionekana yameingiliana kimaana. Kwa hivyo, Waafrika wa kaskazini wa asili ya Kiarabu na KiAmazigh, na ambao hawakuhesabiwa kuwa ni watu “weusi,” hawakuwa na nafasi katika hii dhana ya awali ya Umajumui wa Afrika. Lakini pale Amerika, katika miaka ya 1960 na 1970 pia kulizuka Mvumuko wa Watu Weusi (Black Power), mkondo ambao ulidhihirisha hamu ya Waamerika wa asili ya kiAfrika kupewa heshima kama makabila mengine ya Amerika, hamu ya kuungana na kujitegemea, na baadaye kupigana na ugozi na ubaguzi uliokuwako Amerika. Kwa hivyo mvumuko huu haukuanzisha biashara tu za Waamerika wa asili ya kiAfrika – biashara kama mikahawa, maduka ya vitabu, skuli, zahanati, kampuni za uchapishaji, na kadhalika – kwa nia ya kuendeleza lengo la kujitosheleza, lakini pia tanzu za kimapinduzi kama Black Panther Party (Chama cha Chui Mweusi), zilizokuwa tayari kuchukua silaha na kupigania ukombozi.

Uhuru wa nchi za kiAfrika pia ulichangia katika kukipa Kiswahili msukumo kidogo. Wakiwa na itikadi ya Umajumui wa Afrika, Waamerika wa asili ya kiAfrika wengi sasa walipata fursa ya kwenda Afrika kutembea. Katika safari hizi kulikuwa na bidii za kuunganisha malengo ya uhuru wa Afrika na baadhi ya harakati za Mvumuko wa Watu Weusi zilizokuwa zikiendelea kule Amerika. Tukumbuke kuwa tangu katika miaka ya 1950 tayari kulikuwa na uhusiano baina ya viongozi fulani wa vyama vya kupigania uhuru Afrika waliosomea Amerika – viongozi kama Kwame Nkrumah, Nnamdi Azikiwe na Sibusiso Vil-Nkomo, kwa mfano, waliosomea Chuo Kikuu cha Lincoln (Lincoln University), kimoja katika vyuo vikuu vya kwanza vya Waamerika wa asili

ya kiAfrika au HBCU, yaani Historically Black Colleges and Universities – na baadhi ya viongozi wa Mvumuko wa Watu Weusi.

Lyndon Harries, yule mtaalamu mashuhuri wa masomo ya Kiswahili, alistaajabu sana kuona Waamerika wa asili ya kiAfrika wakichagua Kiswahili kama lugha ya kunadi Uafrika wao. Alistaajabu kwa sababu, kwa maoni yake, Kiswahili ni lugha ya Afrika Mashariki ambayo pia iliwahi kuwa lugha ya utumwa, ya ubwanyenye, na ya usultani wa Zanzibar. Kwa hivyo huko Amerika,

> […] it would seem that the black community has made what at first sight seems a strange choice of this particular African language as a "symbol of pride." Since their forefathers came from west Africa a more logical choice would have been some West African language [… If] the black community in the States wishes to find an African language which represents best what has been most consistently the vehicle of Africa's aspirations and Africa's resistance against foreign domination, Swahili must come very low on the list. (Harries 1968: 146)
>
> […] inastaajabisha kwamba, kwa dhahiri yake, jumuiya ya watu weusi imechagua lugha hii ya kiAfrika kama kitu cha kujivunia. Kwa kuwa mababu zao walitoka Afrika Magharibi lugha inayoingia akilini zaidi ingekuwa ni ile ya Afrika Magharibi. [… Iwapo] jumuiya ya watu weusi wa Amerika inatafuta lugha ambayo ina rekodi ya kuaminika zaidi kama chombo cha matamanio ya Waafrika na mapambano ya Waafrika dhidi ya utawala wa wengine, basi Kiswahili lazima kiwe chini sana katika orodha ya lugha hizo.[1]

Hapa yaonyesha Lyndon Harries alikuwa amesahau nafasi ya Kiswahili katika harakati za ukombozi Tanganyika na miongoni mwa wafanyikazi nchini Kenya. Alikuwa amesahau kwamba Kirusi kilekile cha ubwanyenye wa Urusi ya Tzar, kwa mfano, ndicho kilichokuja kuwa Kirusi cha mapinduzi na ukomyunisti. Alisahau kwamba kwa Waamerika hawa, Afrika haikuwa mgawanyiko wa majimbo na nchi mbalimbali, bali uzao mmoja kamili wa asili yao. Muhimu zaidi, alisahau utendakazi wa Tanzania kama chanzo muhimu cha mwamko huu wa Kiswahili katika siasa za Waamerika wa asili ya kiAfrika.

Katika nchi zote zilizopata uhuru Afrika hakuna iliyokuja kuwa muhimu zaidi katika kuwatia Waamerika wa asili ya kiAfrika ilhamu ya kujifunza Kiswahili kama Tanzania. Tanzania iliwavutia Waamerika wa asili ya KiAfrika kwa sababu nne: (1) Haiba ya Julius Nyerere mwenyewe kama kiongozi wa Afrika, akiwa na hadhi kama ile ya Kwame Nkrumah miongoni mwa Waamerika wa asili ya kiAfrika; (2) Ujamaa, hasa ile dhana ya "kujitegemea" iliyokuwa muhimu katika siasa za Mvumko wa Watu Weusi; (3) Uongozi wa Tanzania katika Umajumui wa Afrika, uongozi ambao uliufanya Mkutano wa Sita wa Chama cha Umajumui wa Afrika ufanyike huko Tanzania katika mwaka 1974; (4) Uongozi wa Tanzania katika kujaribu kuleta ukombozi wa nchi za Afrika – hasa

[1] Tafsiri zote zetu.

Zimbabwe, Msumbiji, Namibia, na Afrika Kusini – ambazo bado zilikuwa chini ya utawala na watu wa asili ya kizungu.

Haya yote ni katika mambo yaliyopatana vizuri, kwa kiwango fulani, na siasa za Mvumko wa Watu Weusi, wa Waamerika wa asili ya kiAfrika hasa katika kipindi hicho cha miaka ya 1960. Hisia na hamu zao za wakati ule sasa zikawapa nguvu Waamerika hawa kuidai na kujivunia asili yao ya kiAfrika. Ndipo Seth Markle alipoandika:

> With African decolonization came the desire, yet the struggle, to connect to and understand Africa's new historical moment and where they [African Americans] fit in a world profoundly being shaped by the formation of new nation-states. Tanzania emerged as one dynamic force that seized the attention of black political activists, extending, deepening, and complicating their relationship with Africa and their conceptions of Pan-Africanism. Between 1964 and 1974, a number of Caribbean and African American nationalists, leftists, and pan-Africanists traveled to and settled in Dar es Salaam to live and work in a nation that many believed was on the forefront of Africa's liberation struggle (Markle 2017: 1-2)

> Pamoja na uhuru wa Afrika, kulikuja ile hamu, pamoja na misukosuko yake yote, ya kujishirikisha na kuifahamu hali mpya ya historia ya Afrika na nafasi yao [Waamerika wa asili yaki Afrika] katika dunia mpya iliyokuwa ikiathiriwa vikubwa na nchi mpya zilizoibuka. Tanzania ilijitokeza kuwa nguvu mpya iliyowavutia sana wana harakati Weusi kwa njia ambayo ilipanua, ikazidisha mizizi, na kuongeza utata uhusiano wao na Afrika na fikra zao juu ya Umajumui wa Afrika. Baina ya 1964 na 1974, Waamerika wa asili ya kiAfrika na WaCaribbean wengi wenye imani za utaifa na Umajumui wa Afrika walitembelea na wakahamia Dar es Salaam kuishi na kufanya kazi katika taifa ambalo wengi waliamini lilikuwa katika hatamu ya mbele ya mapambano ya kuikomboa Afrika.

Na kama viongozi wa Chama cha Siasa Kali cha Watu Weusi (Black Radical Congress) – chama kilichoundwa 1998 kwa lengo la kuendeleza siasa mpya miongoni mwa Waamerika wa asili ya kiAfrika – walivyokiri miaka mingi baadaye, Tanzania iliwakaribisha na kuwapokea vizuri katika miaka hiyo muhimu baina ya 1964 na 1974 (Markle 2017: 179). Na kwa kuwa Kiswahili ndicho kilichokuwa nguzo ya kuwasilisha falsafa ya kimapinduzi ya Tanzania, hakikuwa na budi kukumbatiwa na Waamerika wa asili ya KiAfrika. Tanzania ikikitilia nguvu Kiswahili kama lugha ya taifa na lugha rasmi, "Black Power activists were pushing for the Kiswahili language to be taught in U.S. schools" (Markle 2017: 117) – "wana harakati wa Mvumko wa Watu Wesusi walikuwa wanasukuma Kiswahili kifundishwe katika maskuli ya Amerika." Na kutokana na harakati hizi za Waamerika wa asili ya kiAfrika, Kiswahili kikapanda bei haraka haraka katika vyuo vya Amerika.

Ali Mazrui aliunda neno "Tanzaphilia" kueleza jinsi Tanzania ilivyokuwa kama smaku iliyonasa fikra na mawazo ya wasomi wa nchi za Uzunguzi na wengineo. Kwa maneno ya Mazrui:

> It is to the credit of Tanzania that she had managed to command the varied loyalties and affections of a wide of external admirers. From Gandhians to Maoists, humanitarians to

> ruthless revolutionaries – all these have been known to fall under the soothing spell of Tanzaphilia (1967: 26).
>
> Tanzania inapasa kusifiwa kwa kufaulu kuwavutia na kuwapendeza watu wengi wasiokuwa Watanzania. Tangu wafuasi wa [Mahatma] Ghandhi hadi wa Mao [Tse Tung], watoa misaada kwa msingi wa kibinadamu hadi wanawapinduzi wakali – hawa wote wamevutiwa na mnaso mtamu ya Tanzaphilia.

Na "Tanzaphilia" hii pia ilikuja kuathiri vikubwa mtazamo wa kisiasa wa Waamerika wa asili ya kiAfrika, hasa kuhusu uhusiano wao na bara la Afrika. Mtazamo huo ukawa rutuba muhimu ya masomo ya Kiswahili nchini Amerika.

Kwa Waamerika wa asili ya kiAfrika Kiswahili hakikuwa chombo cha mawasiliano tu, lakini pia kioo cha Uafrika wao. Wengi walivalia mavazi ya Afrika Magharibi kama ishara ya Uafrika wao na wengine walisilimu, wakiamini Uislamu ndio njia ya kudai Uafrika wao waliopokonywa. Lakini kutoka Afrika Mashariki, walichochukua ni Kiswahili; wakakifanya moja ya nguzo muhimu ya kunadi Uafrika wao. Kama alivyosema John Mugane, kwa Waamerika wa asili ya kiAfrika "Swahili has been an inexhaustible resource of symbols of identity […]" (Mugane 2015: 268) - Kiswahili kimekuwa chombo kilichojaa tele alama za kujitambulisha. Washairi, waimbaji, wasomi, na wengineo, wote walijaribu kuchota katika ziwa hili la lugha ya Kiswahili. Na juu ya yote hayo, wakaunda sikukuu yao, *Kwanzaa*, ambayo nguzo zake saba zote zina majina ya Kiswahili na zimejikita katika tamaduni za kiAfrika.

Kabla ya kipindi hiki cha miaka ya 1960 vile vyuo vichache vilivyokuwa vikifundisha Kiswahili – kama Chuo Kikuu cha Indiana au Chuo Kikuu cha Illinois – mara nyingi vilikuwa vikikiweka katika idara za isimu. Katika hali hii, Kiswahili kilifundishwa kama njia moja ya kuwatayarisha wanafunzi wa isimu. Ingawa baadhi ya wanafunzi hawa walimalizikia kuijua na kuitumia lugha yenyewe vizuri, lengo hasa lilikuwa ni kuupanua ujuzi wao wa mambo ya kiisimu. Lakini siasa za Mvumko wa Watu Weusi na mwamko wa Waamerika wa asili ya KiAfrika mara nyingi ulimalizikia kukiweka Kiswahili katika idara za Masomo ya Watu Weusi au ya Waamerika wa Asili ya KiAfrika (Black Studies au African American Studies). Na katika baadhi ya idara hizi, Kiswahili – au lugha nyingine ya Kiafrika – ikawa somo la lazima la kupatia shahada ya BA au MA katika fani hii.

## Kiswahili na Vita Baridi

Jambo la pili lililosaidia kuyapa nguvu masomo ya Kiswahili katika vyuo vya Amerika ni Vita Baridi. Ni wazi kwamba mivutano baina ya Amerika na Usovieti[2] ilianza mapema zaidi kuliko

[2] Tumeunda neno Usovieti kwa maana ya Soviet Union kwa lengo la kuitofautisha na Urusi, Russia

Mvumuko wa Watu Weusi. Lakini kwa bara la Afrika umuhimu wa Vita Baridi ulijitokeza zaidi baada ya nchi zake kuanza kupata uhuru katika miaka ya 1960. Sasa yale mahitaji ya Kiswahili katika siasa za Mvumko wa Watu Weusi, na mahitaji ya Kiswahili katika siasa za Vita Baridi yalikuja kukutana wakati mmoja – katika miaka ya 1960.

Tunajua hasa umuhimu wa Vita Baridi katika kukua kwa Masomo ya Mawanda (Area Studies) Amerika – masomo yaliyotilia mkazo hasa mafunzo ya lugha na tamaduni za majimbo mbalimbali ya dunia. Hivi si kusema kwamba Vita Baridi ndiyo chanzo cha Masomo ya Mawanda, kwani twajua kwamba Masomo ya Mawanda yalianza hata kabla ya vita vya dunia, vya kwanza na vya pili. Lakini ni katika kipindi hiki ambapo malengo ya Masomo ya Mawanda yaliunganishwa kikamilifu zaidi na siasa za dola ya Amerika. Kwa viongozi wengi wa Amerika, basi, hapana shaka kwamba Vita Baridi viliyafanya Masomo ya Mawanda yaingie akilini zaidi na yawafanye viongozi wawe na hamu zaidi kuyapa masomo haya msaada wa serikali (Bundy 2002: 67). Msaada huu ulikuwa chini ya mradi wa Title VI ya Higher Education Act (Kifungu VI cha Sheria ya Elimu ya Juu) ya 1965, yaani mradi wa International Foreign Language Education (Elimu ya Kimataita ya Lugha za Kigeni) wa Idara ya Elimu uliokusudiwa kutilia nguvu ufundishaji wa "lugha za kigeni" na Masomo ya Mawanda (Area Studies) na Masomo ya Kimataifa (International Studies). Na hivi ndivyo Masomo ya Afrika (African Studies), kama moja ya tanzu za Masomo ya Mawanda yalivyopata nguvu zaidi Amerika, huku yakikipanulia nafasi Kiswahili katika vyuo vya Amerika.

Kama nchi nyingine nyingi ulimwenguni, nchi za Afrika Mashariki nazo zilikuwa uwanja wa mapambano baina ya Amerika na Usovieti. Na kama siasa za Afrika Mashariki zilivyoathiri msimamo wa Mvumko wa Watu Weusi katika vita vyake na Watu Weupe, ndivyo pia zilivyokuja kuathiri msimamo wa Amerika katika vita vyake na Usovieti. Kutokana na mivutano ya mataifa mawili haya, ujuzi wa Kiswahili ukathaminiwa kwa sababu ya mahitaji ya propaganda za kisiasa na kiitikadi.

Lakini kulikuwa na maendeleo gani ya kisiasa kule Kenya, Tanzania na Uganda, yaliyolifanya jimbo hili nalo liwe moja ya nyanja za Vita Baridi? Kwa hakika kila nchi ya Afrika Mashariki ilikuwa na mambo yake. Kwa upande wa nchi ya Kenya kulikuwa na ule mgongano baina ya viongozi wa chama cha KANU (Kenya African National Union) – akina Jomo Kenyatta, Tom Mboya na wenzao – kwa upande mmoja, na viongozi wa chama kipya cha KPU (Kenya People's Union) – akina Jaramogi Oginga Odinga, Bildad Kaggia na wenzao – kwa upande mwingine. Mgongano huu ulikuwa mgongano wa kiitikadi, KANU ikiwa imemili upande wa ubepari, na KPU upande wa kiujamaa. Bila ya shaka basi, Amerika ilijitokeza kwa nguvu kusimama na KANU. Na hapana maandishi yaliyodhihirisha kwa uwazi zaidi msimamo wa Amerika kuhusu siasa za Vita Baridi nchini Kenya kama kitabu cha balozi wake wa kwanza wa Kenya, William Attwood, yaani *The Reds and the Blacks* (1967). Hadithi ya Attwood ni hadithi ya ukora wa Amerika hasa, ya

mbinu chafu zilizotumiwa kuhakikisha kuwa Kenya haitaingia katika kambi ya Usovieti au ya Uchina.[3]

Amerika iliichukulia hamu Tanzania hata kabla Ujamaa kuanzishwa. Wasiwasi mkubwa wa Amerika ulitokana na mapinduzi ya Zanzibar ya 1964. Chini ya uongozi wa watu kama Abdulrahman Babu na "makomredi" wenzake waliokuwa na fungamano kubwa na Cuba, ilikuwa wazi kwamba mapinduzi ya Unguja yalidhamiria kuleta ukomyunisti pale kisiwani. Hata inasemekana kwamba kwa kiasi fulani muungano wa Tanganyika na Zanzibar uliozaa Tanzania ulitokana na njama za CIA za kuhakikisha kwamba Zanzibar haitakuwa nchi ya kikomyunisti (Wilson, 1989). Amerika ilikuwa tayari kuishi na Ujamaa wa Tanzania; lakini haikuwa tayari kuiona Zanzibar ikiibuka na kuwa Cuba mpya katika mwambao wa Afrika Mashariki.

Kama tunavyokumbuka, mapinduzi haya yalikuwa na umuhimu mkubwa katika kukieneza Kiswahili sehemu ya nchi za Arabuni. Wengi katika wasemaji wa Kiswahili wa Unguja na Pemba walilazimika kutoroka, na wengi wao walimalizikia kuanzisha maisha mapya Oman na baadaye katika nchi za Imarati (Emirates). Lakini inaonekana vizazi vya "muhajirina" hawa havitaweza kukiendeleza Kiswahili katika sehemu hii ya dunia, kwani wengi wao sasa wanaenukia wakisema Kiarabu.[4]

Katika miaka yake ya kwanza baada ya uhuru, Uganda haikuitia Amerika wasiwasi wowote kwamba inaweza kuingia katika kambi ya ukomyunisti na kuwa pamoja na Usovieti. Lakini katika mwaka 1969, rais wake, Milton Obote alifaulu kupitisha sheria mpya iliyotokana na ule waraka wake wa *Common Man's Charter: First Steps for Uganda to Move to the Left* wa chama chake cha UPC (Uganda People's Congress). Bila ya shaka matokeo haya yalisababisha wasiwasi mkubwa miongoni mwa CIA. Lakini kama tujuavyo, miaka miwili baadaye serikali ya Obote ilipinduliwa na Idi Amin Dada. Kuna wasemao kwamba mapinduzi haya yalipata msaada wa Amerika, Israel na Uingereza (Mamdani 1983), na kwamba mapinduzi yenyewe yalisababishwa vikubwa na hilo lengo la kisiasa la kuelekea za mkondo wa kushoto.

Kwa jumla basi baina ya kupata uhuru na miaka ya 1970, siasa za nchi zote za Afrika Mashariki zilionyesha kwamba jengo la mfumo wa kibepari lililosimamishwa na wakoloni limo hatarini. Hili likawa moja katika sababu muhimu ya Amerika kujaribu kuzitawala na kuziendesha siasa za nchi

---

[3] Wakati huohuo, Amerika ilikuwa haitaki kuweko na uhusiano baina ya viongozi wa Kenya na viongozi wa Black Power kule Amerika. Attwood, kwa mfano, anaeleza kisa kilichotokea Malcom X alipokuja kutembea na kukutana na viongozi wa Kenya. Anasimulia namna alivyofanya kila njama ili Malcolm X atolewe Kenya, arudishwe Amerika, na namna gani alivyofaulu katika lengo lake hili.

[4] Profesa Salah Hassan, Mkurugenzi wa Taasisi ya KiAfrika, Sharjah, ana mpango wa kuanzisha na kufundisha Masomo ya Kiswahili kwa lengo la kuiendeleza lugha hii miongoni mwa wananchi wa UAE.

za Afrika Mashariki, na moja katika sababu muhimu ya kutaka Kiswahili kifundishwe katika vyuo vyake. Sababu zilizofungamana na Vita Baridi na sababu zilizofungamana na Mvumuko wa Watu Weusi), zote zikiwa na malengo ya kitaifa na ya kimataifa, sasa ziliingiliana kwa njia fulani iliyokipa Kiswahili msukumo mkubwa nchini Marekani.

Tofauti moja iliyokuwepo katika malengo ya Mvumko wa Watu Weusi na Vita Baridi ni ile ya idara itakayokisimamia Kiswahili. Siasa za Mvumko wa Watu Weusi zilipendelea Kiswahili kifundishwe kama ala ya ukombozi katika idara za Masomo ya Watu Weusi, na zile za Vita Baridi, kifundishwe kama somo la vituo vya Masomo ya Kiafrika kwa lengo la utawala. Lakini mgawanyiko huu wa idara mara nyingi ulikuwa hauwezekani, hasa kwa kuwa Mvumuko wenyewe wa Watu Weusi uliyachukulia Masomo ya Afrika kuwa ni pamoja na Masomo ya Watu Weusi kwa jumla. Yaani kwa wengi Masomo ya Watu Weusi yalikuwa yanachanganya Masomo ya Waamerika wa Asili ya kiAfrika na Masomo ya Afrika.

Kundi kubwa la Waamerika ambalo lilijifunza Kiswahili katika muda huu wa Vita Baridi ni lile la Peace Corps Volunteers waliopelekwa Kenya na Tanzania. Peace Corps yenyewe ilianzishwa kutokana na hofu ya kwamba Usovieti imeingia kusaidia mataifa mbalimbali ulimwenguni na, kwa njia hii, ikaweza kueneza itikadi yake. Sasa Peace Corps iliundwa kama chombo cha kusaidia kueneza itikadi ya Amerika. Kwa maneno mengine, Peace Corps

> […] was an outgrowth of the Cold War. President Kennedy pointed out that the Soviet Union 'had hundreds of men and women, scientists, physicists, teachers, engineers, doctors, and nurses […] prepared to spend their lives abroad in the service of the world of communism.' The United States had no such program, and Kennedy wanted to involve Americans more actively in the cause of global democracy, peace, development, and freedom.[5]

> […] ilitokana na Vita Baridi. Rais Kennedy alieleza kwamba 'Usovieti ilikuwa na mamia ya watu waume kwa wake, wana-sayansi, wana-fizikia, waalimu, wahandisi, madaktari, wauguzi […] wote wakiwa tayari kujitolea kuishi ng'ambo wakiutumikia ulimwengu wa kikomyunisti.' Amerika haikuwa na mpango kama huo, na Kennedy alitaka kuwashirikisha Waamerika zaidi katika kuitumikia demokrasia duniani, amani, maendeleo, na uhuru.

Kutokana na mradi huu mpya wa serikali ya Amerika, na kwa sababu Waamerika wengi walihitari kujiunga na Peace Corps kuliko kupelekwa Vietnam kupigana, maelfu ya Waamerika wa asili mbalimbali walipata fursa ya kujifunza Kiswahili.[6] Kipande kidogo cha hadithi hii ya Peace Corps

---

[5] Tazama mada ya "Peace Corps" katika mtandao wa John F. Kennedy Presidential Library and Museum. https://www.jfklibrary.org/learn/about-jfk/jfk-in-history/peace-corps (mara ya mwisho kufunguliwa tarehe 25-03-2021).

[6] Baadhi ya Waamerika waliorudi kutoka Peace Corps hata walikata kurudi chuoni na kujifunza isimu, na walipohitimu baadhi yao wakawa waalimu wa isimu na Kiswahili katika vyuo na maskuli ya Amerka.

ni kile kilichoelezwa vizuri katika filamu ya 2020 ya David Asher Goldenberg, *Swahili on the Prairie.*

Katika Usovieti nako, Vita Baridi vilikuwa na athari kama ile iliyokuwako Amerika kwa kiasi fulani. Kweli, Masomo ya Kiafrika kwa jumla yalianza tangu miaka ya 1930. Lakini, pamoja na masomo ya Kiswahili, yalipata kasi zaidi kuanzia miaka ya 1960. Hapa ndipo Usovieti ilipoanza kuingia katika uwanja wa siasa za Afrika, ikipinzana na Amerika. Baadhi ya vitabu vya Kiswahili vilitafsiriwa kwa Kirusi ili Warusi wenyewe wapate kufahamu hali na tamaduni za Afrika (Gromov 2018: 165). Lakini, Usovieti pia ilitafsiri baadhi ya kazi za Kirusi kwa Kiswahili, kama riwaya ya Maxim Gorky, *Mother*, na vitabu vingine visivyokuwa vya fasihi, kwa lengo la kuingiza itikadi yake ya kikomyunisti katika siasa za Afrika Mashariki, kama Amerika ilivyofadhili tafsiri ya riwaya ya George Orwell, *Animal Farm* kwa lugha mbalimbali duniani kwa lengo la kuipinga itikadi ya Usovieti na kuitilia nguvu itikadi yake ya kibepari.

## Kiswahili baada ya Vita Baridi na Mvumko wa Watu Weusi

Lakini tukiingia katika miaka ya 1990 na kuendelea, tunashuhudia mabadiliko makubwa ya kisiasa ulimwenguni. Kwanza ni kumalizika kwa Vita Baridi. Kwa mtaalamu kama Francis Fukuyama, mwisho wa Vita Baridi na wa Usovieti kama tulivyokuwa tukiijua, ulikuwa pia mwisho wa historia ya migongano ya kiitikadi. Ubepari na dhana ya demokrasia ya nchi za Magharibi sasa zilipata ushindi kamili tena wa kudumu (Fukuyama 1992). Tukubaliane au tusikubaliane na Fukuyama, lililo wazi ni kwamba mwisho huu wa Vita Baridi pia uliifanya serikali ya Amerika isiwe na hamu tena ya kusaidia kifedha Masomo ya Afrika/Masomo ya Mawanda na lugha zake kama vile zilivyokuwa zikifundishwa zamani.

Pili, Afrika ilipungua mvuto wake kama dhana, kama shina la itikadi ya kisiasa kwa Waamerika wa asili ya kiAfrika. Hili lilisababishwa na mambo manne au matano hivi. Kwanza barani Afrika mwelekeo wa Umajumui wa Afrika ulianza kubadilika. Lengo lake likawa silo tena kuunganisha na kupigania haki za watu wote wa asili ya kiAfrika duniani (trans-continental Pan-Africanism), bali la kuleta muungano na kusaidia maendeleo ya nchi za bara la Afrika peke yake (continental Pan-Africanism). Mabadiliko haya bila ya shaka yalikuwa na athari ya kuwatenga Waamerika, Waingereza, Wafaransa na watu wengine duniani wenye asili ya kiAfrika.

Kwa miaka kadhaa, Waamerika wa asili ya kiAfrika waliendelea kujishughulisha na harakati na maendeleo ya Afrika, hata wakionyesha kutaka kusaidia kwa njia mbalimbali. Siasa za Afrika Kusini zilikuwa muhimu katika maoni yao. Hiki kilikuwa kipindi ambacho Afrika Kusini bado ilikuwa katika utawala wa Makaburu. Sheria za ugozi (za Apartheid) zilikuwa zimefanana vizuri na zile sheria za Jim Crow katika historia ya Waamerika wa asili ya kiAfrika. Lakini baada ya Nelson Mandela kufunguliwa, na Afrika Kusini kuanza kufuata mfumo wa kidemokrasia uliompa

kila mwananchi kura sawa na mwengine, mshipa wa kitovu uliokuwa ukiendelea kuwaunganisha Waamerika wa asili na kiAfrika na wenyeji wa bara la Afrika lenyewe, ukazidi kudhoofika.

Kwa upande mwingine, kama tulivyotangulia kueleza, Waamerika wengi wa asili ya kiAfrika walipata fursa ya kutembelea nchi mbalimbali za bara la Afrika baada ya kupata uhuru. Mwanzoni ziara hizi zilizidisha hamu yao ya kujinasibisha na Uafrika. Lakini kila miaka ikipita, Waamerka wa asili ya kiAfrika wengi waliowahi kuzuru au kuishi Afrika walitanabahi kwamba kuna tofauti kubwa baina yao na Waafrika wenzao wa barani. Wengi walianza kuamini kwamba ingawa wao wana asili ya kiAfrika, utamaduni wao, mwelekeo wao, mila na desturi zao nyingi, zilidhihirisha kwamba wao ni Waamerika kindakindaki. Ikiwa kwa baadhi ya miaka baada ya uhuru walikuwa wakijaribu kuupa uzito Uafrika wao, sasa wakawa wanaupa uzito zaidi Uamerika wao. Na hata watu mashuhuri kama Morgan Freedman na Saidiya Hartman wamejitokeza waziwazi kusema kwamba wao si Waafrika kamwe; ni Waamerika tu.

Kisha kuna athari za hivi karibuni zaidi nchini Amerika, athari za wahamiaji kutoka Afrika na Caribbean. Kutokana na sababu zilizofungamana na utandawazi, Waafrika na WaCaribbean wengi kutoka sehemu mbalimbali wamehamia na kuanzisha makazi na maisha yao Amerika. Kama Berlin anavyoeleza,

> Before 1965, black people of foreign birth residing in the United States were nearly invisible. According to the 1960 census, their percentage of the population was to the right of the decimal point. But after 1965, men and women of African descent entered the United States in ever-increasing numbers. During the 1990s, some 900,000 black immigrants came from the Caribbean; another 400,000 came from Africa; still others came from Europe and the Pacific rim. By the beginning of the 21st century, more people had come from Africa to live in the United States than during the centuries of the slave trade. At that point, nearly one in ten black people was an immigrant or the child of an immigrant. (2010)

> Kabla ya 1965, watu weusi nchini Amerika waliozaliwa ng’ambo walionekana kwa nadra sana. Kwa mujibu wa sensa ya 1960, idadi yao ilikuwa hata haifiki asilimia moja. Lakini baada ya 1965 Waafrika wanaume na wanawake walianza kuingia Amerika kwa idadi iliyokuwa haiachi kuongezeka. Katika miaka ya 1990, kulikuwa na wahamiaji kama 900,000 kutoka Caribbean; na wengine 400,000 kutoka Afrika; na wengine zaidi walikuja kutoka Ulaya na nchi zilizopakana na Bahari ya Pacific.Tukiingia mwanzo wa karne ya 21, kulikuwa na watu zaidi kutoka Afrika waliokuja kuishi Amerika kuliko wa karne zote za utumwa. Hapo basi, takriban mtu mweusi mmoja katika kila kumi alikuwa anatoka ng’ambo au mtoto wa wazazi waliotoka ng’ambo.

Kila idadi yao ikiongezeka, uhusiano baina ya wahamiaji hawa na Waamerika wa asili ya kiAfrika umezidi utata. Maingiliano yao ya kila siku yakawa kama kioo kilichowapa Waamerika wa asili ya kiAfrika kujitazama mara mbilimbili, na kujifahamu upya kwa njia ambayo kila uchao ilizidi kuutokeza Uamerika wao.

Vile Waamerika wa asili ya kiAfrika wanavyojiona, wanavyojitambulisha, pia iliathiri siasa zao. Tukiingia katika miaka ya 1980 na kuendelea, mkazo sasa ulimili zaidi upande wa kupigania haki na usawa – katika nyanja za siasa, uchumi, na jumuiya kwa jumla – kama Waamerika sawa na Waamerika wengine. Na mabadiliko yote haya yalipunguza mvuto wa Afrika, na kwa hivyo mvuto wa Kiswahili, kama kimoja katika viini vya siasa za Waamerika wa asili ya kiAfrika.

Ni kweli kwamba hivi sasa kuna mwamko mpya wa siasa za Waamerika wa asili ya kiAfrika, mwamko wa "Maisha ya Weusi ni Muhimu" (Black Lives Matter au BLM) ambao pia umesisimua ari ya kisiasa ya watu wa asili ya kiAfrika na wengineo katika nchi mbali mbali duniani. Lakini mwamko huu ni katika hizi siasa mpya ambazo zinajishughulisha zaidi na mambo ya "ndani" tu nchini Amerika bila ya fungamano dhahiri na Afrika. Baada ya mauaji ya Mei 2020 ya George Floyd hasa, BLM ilisisimua hisia za kisiasa za watu wengi wa asili ya kiAfrika na wengineo katika sehemu nyingi duniani nje ya Amerika. Lakini tukio hili la utandawazi halikusaidia katika kuamsha upya hisia na siasa za kujinasibisha na Afrika miongoni mwa Waamerika wa asili ya kiAfrika.

Sasa, ikiwa Vita Baridi baina ya Amerika na Usovieti vimemalizika, na ikiwa siasa za Waamerika wa asili ya kiAfrika zimebadilika na sasa zinajishughulisha zaidi na hali ya mambo nchini Amerika kuliko uhusiano wao na Afrika, nini mwelekeo wa Kiswahili Amerika? Tuseme masomo ya Kiswahili sasa hayana tena tamaa ya kuendelea Amerika?

Tunafahamu kwamba tangu zamani kuna Waamerika wengi waliojifunza na wengine wanaoendelea kujifunza Kiswahili kwa malengo ya kibinafsi kabisa ambayo hayahusiani na Vita Baridi wala siasa za Mvumko wa Watu Weusi. Katika madarasa ya Kiswahili ya vyuo vingi Amerika tumeona wanafunzi waliotaka kujifunza Kiswahili kwa sababu za mahitaji ya utafiti, za kuhubiri "Neno la Mungu," za kutembea kwa utalii, na hata za mapenzi na ndoa. Lakini vyuo vingi ambavyo havipati msaada wa serikali, kama ule wa Kifungu VI (Title VI), kwa mfano, huwa havikubali kuendelea kufadhili masomo ya Kiswahili na masomo mengi mengineyo iwapo hakuna "idadi ya kutosha" ya wanafunzi wanaojifunza masomo hayo. Huona haihalisi kuendelea kufundisha masomo kama hayo. Na kwa maoni yetu, hakuna wanafunzi wenye sababu za kibinafsi za kujifunza Kiswahili kwa "idadi ya kutosha" ya kuweza kuhakikisha kwamba vyuo visivyopata msaada wa serikali vitakuwa tayari kuendelea kuyafadhili masomo ya Kiswahili. Basi tunarudia tena lile swali letu: Masomo ya Kiswahili nchini Amerika yatakuwa na maisha gani baada ya Vita Baridi na siasa za Mvumko wa Watu Weusi?

Inavyonekana mpaka sasa ni kwamba Kiswahili kitaendelea kufundishwa katika baadhi ya vyuo ambavyo vinawalazimu wanafunzi kujifunza angalau lugha moja ya "kigeni". Kuna vyuo vingi Amerika ambavyo bado vina sharti hii ya kujifunza lugha ya kigeni kabla ya mwanafunzi hajakubaliwa kuhitimu shahada ya kwanza. Iwapo Kiswahili ni mojawapo wa lugha

zinazofundishwa katika vyuo hivi, basi wanafunzi wengi huweza kukichagua kwa lengo la kutekeleza sharti hii. Katika vyuo vikuu vinavyotajika zaidi na ambavyo vina masomo ya Kiswahili ni kama Princeton, Yale, Pennsylvania, Columbia, Cornell, Tufts, North Carolina-Chapel Hill, na kadhalika. Pia kuna vyuo, kama Harvard, Massachusetts Institute of Technology (MIT), Stanford, John Hopkins, Chicago, Wesleyan, Bryn Mawr, na vinginevyo ambavyo, ingawa "lugha ya kigeni" si somo la lazima, vina utajiri wa kutosha wa kuendelea kufundisha Kiswahili hata ikiwa idadi ya wanafunzi darasani ni ndogo sana. Na baadhi ya vyuo ambavyo kihistoria ni vya Waamerika wa asili ya kiAfrika – kama Howard, Lincoln, Morgan State, Delaware State, Morehouse na Norfolk State – Kiswahili pia kinaendelea kufundishwa kwa kiwango fulani.[7]

Juu ya haya yote, hapana shaka kwamba nguvu ya masomo ya Kiswahili imepungua sana tangu miaka ya sitini, sabini na themanini. Basi je, nje ya vyuo tulivyovitaja hapo juu, Kiswahili kitakuwa na maisha ya aina gani nchini Amerika baada ya Mvumko wa Watu Weusi na Vita Baridi? Tuna hakika hakitafifia kabisa kabisa. Lakini je, kinaweza kudhoofika kikafika daraja ya kutotajika tena miogoni mwa lugha muhimu za kigeni za dunia zinazofundishwa katika vyuo vya Amerika?

## Kiswahili katika Siku Zijazo

Kwa hakika, kuna matokeo mawili matatu ya hivi karibuni ambayo pengine huenda yakawa sababu ya Kiswahili kuendelea kuwa na nafasi katika vyuo vya Amerika. La kwanza ni mvutano baina ya Amerika na Uchina – mvutano ambao wengine wameuita Vita Baridi vya pili. Hii ndiyo mada hasa ya kitabu kipya cha Ashley Tellis na wenzake, *US-China Competition for Global Influence* (Tellis, Szalwiski & Wills 2020), na maandishi mengi mengine ya hivi karibuni. Lakini tofauti na Vita Baridi baina ya Amerika na Usovieti, huu mgongano baina ya Amerika na Uchina haukujikita katika tofauti za kiitikadi, bali unatokana na mashindano ya kiuchumi na kiteknolojia yanayoendelea kila sehemu duniani, pamoja na ile ya nchi za Afrika Mashariki. Leo Uchina imekuwa mtambo wa utandawazi unaoshindana na Amerika kwa nguvu zake. Lakini mpaka sasa haioneshi kwamba Amerika inaitakidi kwamba ujuzi wa Kiswahili ni muhimu katika kuweza kupata ushindi wa kiuchumi dhidi ya Uchina katika jimbo la Afrika Mashariki, ingawa baadhi ya vyuo vinahimiza ufundishaji wa lugha kwa shughuli maalum – language for special purposes – kama Kiswahili kwa Biashara (Swahili for Business) na kadhalika.

[7] Tazama "Naming the American Universities With the Most Extensive Courses in African Languages," katika *The Journal of Black in Higher Education*, 2005. https://www.jbhe.com/news_views/46_africanlanguages_uni.html (mara ya mwisho kufunguliwa tarehe 21-05-2021).

Pengine lugha inayoonekana muhimu zaidi nchini Amerika kwa mashindano haya ni Kichina chenyewe. Hapana shaka ya kwamba wanafunzi wengi wanahimizwa kujifunza Kichina, si katika vyuo vikuu tu, bali hata katika shule za msingi na za sekondari. Kwa mujibu wa taarifa moja:

> Chinese language courses are now available in primary and secondary schools in Washington D.C. and every U.S. state except South Dakota, ranks it the fourth most widely taught foreign language in the country's education system, according to a national survey released Thursday.[8]

> Masomo ya lugha ya Kichina sasa yanapatikana katika shule za msingi na sekondari pale Washington D.C, na katika kila jimbo la Amerika, isipokuwa South Dakota, Kichina kinahesabika kuwa lugha ya nne katika lugha za kigeni zinazofundishwa zaidi katika elimu ya taifa, kwa mujibu wa utafiti uliotoka Alhamisi.

Ingawa wengi katika wanafunzi hawa ni wale wa asili ya Kichina, kumekuwa na maongezeko makubwa ya Waaamerika wanaojifunza Kichina. Baina ya 2009 na 2015, kwa mfano, idadi yao iliongezeka maradufu.[9] Na katika mradi wao wa "One Million Strong" (Nguvu za watu milioni) Rais wa Amerika, Barrack Obama, na Rais wa Uchina, Xi Jinping, walikusudia kuleta maongezeko makubwa sana ya wanafunzi wa Amerika wa shule za msingi na sekondari wanaojifunza Kichina (cha lahaja ya Kimandarin, hasa).[10]

Kwa upande mwingine, mashindano haya huenda yakaathiri zaidi masomo ya lugha kule Uchina kuliko Amerika, kwa sababu mbili. Lugha kuu ya Amerika ni Kiingereza, lugha ambayo inatumika sana katika nchi zote za Afrika Mashariki. Kwa kiasi kikubwa basi, viongozi wa ulimwengu wa biashara wa Amerika hawajioni kama wanahitaji Kiswahili kuwasiliana, kukubaliana, na kuandikiana mikataba na viongozi wa biashara wa Afrika Mashariki. Lakini lugha kubwa ya Uchina si lugha inayotumika sana Afrika Mashariki na nchi nyingi nyingine duniani kwa viwango mbali mbali. Kwa sababu hii, Uchina imemalizikia kutumia mbinu tatu za kujaribu kujenga mawasiliano ya kilugha na nchi za Afrika Mashariki, na kwengineko. Moja ni kujaribu kuwafundisha watu wengine lugha ya Kichina na utamaduni wake – kazi hii imekuwa mradi mkubwa wa Taasisi za Confucius ambazo zimeenea duniani. Pili ni kuwafundisha Wachina

---

[8] Tazama *Popularity of Chinese language learning soaring within the US education system Survey*. http://www.xinhuanet.com/english/2017-06/03/c_136336004.htm (mara ya mwisho kufunguliwa tarehe 21-05-2021).

[9] Tazama *The National K-12 Foreign Language Enrollment Survey*, American Councils for International Education, 2017. Hii ni ripoti ya utafiti uliofadhiliwa na The Language Flagship at the Defense Language and National Security Education Office. https://www.americancouncils.org/sites/default/files/FLE-report-June17.pdf (mara ya mwisho kufunguliwa tarehe 21-05-2021).

[10] Tazama *America's Languages: Investing in Language Education for the 21st Century*, Mradi wa Commission on Language Learning wa American Academy of Arts and Sciences. https://www.amacad.org/sites/default/files/publication/downloads/Commission-on-Language-Learning_Americas-Languages.pdf (mara ya mwisho kufunguliwa tarehe 21-05-2021).

Kiingereza kama lugha ya kimataifa, somo ambalo kila uchao linaonesha kushika kasi katika maskuli na vyuo vya Uchina. Na tatu ni kupata Wachina ambao wako tayari kujifunza lugha, kama Kiswahili, ya nchi au jimbo maalum ambalo lina umuhimu wa kiuchumi na kibiashara kwa Uchina. Tayari Kiswahili kilikuwa kinafundishwa Beijing na pengine kwengineko nchini China; lakini sasa nafasi yake yaonyesha kupanuka. Katika mwaka wa 2019, kwa mfano, Shanghai International Studies University (Chuo cha Masomo ya Kimataifa cha Shanghai) ilianzisha masomo ya shahada ya kwanza (BA) ya Kiswahili kwa lengo la kuwa na Wachina ambao watakuwa na ujuzi wa kutosha wa lugha hii wa kuweza kuyaendeleza maslahi ya Uchina katika nchi za Afrika Mashariki.[11]

Tofauti nyingine muhimu baina ya Amerika na Uchina ni kwamba katika nchi za Afrika Mashariki, biashara za Amerika ni zile kubwa kubwa tu ambazo zinaendeshwa na viongozi na wakurugenzi wa makampuni makubwa. Lakini biashara za Uchina barani Afrika si za serikali na makampuni makubwa tu. Kuna Wachina wengi ambao wameanzisha makazi yao Afrika, wengi wakifanya biashara ndogo ndogo za kibinafsi. Chembelecho Howard French:

> By common estimate, Africa has received millions of […] Chinese newcomers in the space of a mere decade, during which time they have rapidly penetrated every conceivable walk of life: farmers, entrepreneurs building small and medium-sized factories, and practitioners of the full range of trades, doctors, teachers, smugglers, prostitutes. (2014: 5)

> Kwa idadi ya kukisia, Afrika imepata mamilioni […] ya wahamiaji wa KiChina kwa kipindi cha muongo mmoja tu, wakati ambapo waliweza kuingilia takriban aina zote za kazi za kupatia maishilio: wakulima, wajasiriamali waliojenga viwanda vidogo na vya kiasi, na weledi wa kila aina ya kazi – matabibu, waalimu, wafanya magendo, malaya n.k.

Nyingi katika hizi ni kazi na biashara ambazo zinawalazimisha Wachina hawa kuingiliana na wananchi wa kawaida, maingiliano ambayo hatimaye yanawasaidia kujifunza lugha za kiAfrika kama Kiswahili na nyinginezo. Na tunadhani kila inavyozidi idadi ya Wachina hawa wa ng'ambo, wa Afrika Mashariki hasa, ndivyo Uchina yenyewe itakavyozidi kukipa Kiswahili umuhimu katika vyuo vyake.

Sasa ingawa Vita Baridi na Uchina havionyeshi tamaa ya kuwahimiza Waamerika kujifunza Kiswahili, kuna vita vingine ambavyo tayari vimekipa Kiswahili umuhimu mpya katika mipango ya serikali. Na hivi ni vile vilivyotokana na tuhuma na utesi wa Amerika na ulimwengu wa Waislamu. Kama tujuavyo, Usovieti ilipomalizika kuporomoka tu, Amerika ilianza kuulenga Uislamu kama adui yake mpya. Kwa maneno ya John Woods, yule profesa maarufu wa historia ya Mashariki ya Kati, "Almost immediately after the collapse of Communism, Islam emerged as the

[11] Tazama Tanzania: Chinese University Embraces Kiswahili, iliyotoka katika *Daily News* ya Tanzania, 12 June, 2019. https://allafrica.com/stories/201906120583.html (mara ya mwisho kufunguliwa tarehe 06-03-2021).

new evil force" – Vile ukomyunisti ulivyokwisha kuporomoka tu, Uislamu ukachukuliwa kuwa adui mwovu mpya – katika mawazo ya dola ya Amerika.[12] Hapa ndipo ilipopitishwa Sheria ya David L. Boren ya Usalama wa Taifa (the David L. Boren National Security Act), na hasa ule mradi wake mkubwa, Mpango wa Elimu wa Usalama wa Taifa (National Security Education Program au NSEP) ambao lengo lake kubwa ni "To provide the necessary resources […] to meet the national security education needs of the United States […]"[13] – Kutoa msaada unaohitajika […] kusaidia mahitaji ya kielimu ya usalama wa kitaifa wa Amerika. Dola ya Amerika sasa ikaanza kutilia mkazo ufundishaji wa lugha za Waislamu duniani, Kiswahili kikihesabiwa kama mojawapo ya lugha hizo.

Baadaye tena kukazuka vita dhidi ya ugaidi katika sehemu za Afrika Mashariki na kwingineko. Mashambulio ya 1998 ya ofisi za ubalozi wa Amerika nchini Kenya na Tanzania, ya Paradise Hotel (Kikambala) katika mwaka 2002, na mengineyo, yote yalionekana kuwa na fungamano na historia moja na mashambulio ya 2001 ya Twin Towers, New York. Ndipo bunge la Amerika lilipopitisha Sheria ya Masomo ya Kimataifa ya Elimu ya Juu (the International Studies in Higher Education Act (HR 3077) katika mwaka 2003 ambayo, kama Kifungu VI/Title VI (Elimu ya Kimataifa ya Lugha za Kigeni/International Foreign Language Education) ya kipindi cha Vita Baridi, "sought to tie federal funding for university-based area studies programs to the interests of US security state" (Paik 2013: 3) – ilijaribu kuunganisha mpango wa serikali wa kusaidia Masomo ya Mawanda vyuoni na yale maslahi ya usalama wa Amerika. Lakini usalama (security) sasa ulitazamwa kwa mintaarafu ya "magaidi wa Kiislamu" badala ya maadui wa Vita Baridi. Na serikali ya Amerika ikawacha kuzingatia lugha ambazo zilikuwa zimefungamana na Vita Baridi, na kuanza kutilia mkazo lugha za ulimwengu wa Waislamu.

Kama tujuavyo ule mpango wa Kifungu VI ulikuwa chini ya Idara ya Elimu ya Amerika. Lakini mpango mpya sasa, ule wa NSEP (National Security Education Program/Mpango wa Elimu wa Usalama wa Taifa) hasa, ukawa chini ya Idara ya Ulinzi (Department of Defence). Mradi mmoja muhimu wa NSEP ni ule wa African Language Flagship Program, mradi ulio na lengo la kusaidia wanafunzi wa kiAmerika kujifunza na kupata ujuzi mkubwa wa zile "critical languages," yaani "lugha muhimu zaidi" za Afrika, Kiswahili kikiwa hatamu ya mbele kabisa, kwa usalama wa Amerika. Kuanzia hapo basi, Kiswahili na baadhi ya lugha nyingine za Waislamu, zimekuwa pia zikifundishwa kulingana na malengo ya fani mpya ya Masomo ya Usalma (Security Studies).

---

[12] *The New York Times*, August 28, 1995.

[13] Tazama mtandao wa NSEP: https://www.nsep.gov/content/mission-and-objectives (mara ya mwisho kufunguliwa tarehe 14-04-2023).

Umuhimu unaopewa Masomo ya Usalama nchini Amerika hivi leo hauwezi kutenganishwa na fikra za Samuel Huntington alizozitoa katika kitabu chake *The Clash of Civilizations.* Kama tunavyokumbuka, Huntington ameeleza kwamba baada ya Vita Baridi kumezuka vita vipya ambavyo msingi wake ni utamaduni na dini, badala ya itikadi za kisiasa. Ameeleza kwamba "The years after the Cold War witnessed the beginnings of dramatic changes in people's identities and the symbols of those identities. Global politics began to be reconfigured along cultural lines" (Huntington 1996: 19) – Katika miaka iliyofuatia Vita Baridi tulishuhudia mabadiliko makubwa katika ujitambulishaji wa watu na ishara zake. Siasa za dunia sasa zilianza kuchukua mkondo wa kitamaduni. Na katika tamaduni au staarabu zote duniani, kwa maoni ya Huntington, hakuna ambazo zina hatari kubwa zaidi ya kugongana kuliko zile za Wazungu, kwa upande mmoja, na Waislamu, kwa upande mwingine. Na fikra hii ilikuja kukipa Kiswahili, kama Kiarabu na lugha nyingine za Waislamu duniani, umuhimu fulani katika fikra za wakuu wa dola ya Amerika kuhusu usalama wa nchi yao.

Jambo la tatu ambalo huenda likaathiri hali ya masomo ya Kiswahili Amerika ni maongezeko makubwa sana ya Waafrika muhajirina. Ikiwa umuhimu wa Kiswahili Amerika kwanza ulifungamana na historia ya Waafrika wahamiaji (Diaspora) wa kale, maendeleo yake hivi leo yanaweza kutegemea Waafrika wahamiaji waliowasili Amerika katika miongo ya hivi karibuni. Zamani madarasa ya Kiswahili katika vyuo vingi vya Amerika yalikuwa yamejaa Waamerika wa asili ya Kiafrika. Siku hizi, kila uchao, tunaona idadi ya watoto na wajukuu wa Waafrika wahamiaji wapya ikiongezeka katika madarasa haya. Wengi huwa wamezaliwa Amerika au wamekuja Amerika wakiwa wadogo sana. Hawa ni katika wale ambao Ali Mazrui aliwaita siyo *African Americans*, lakini *American Africans* – yaani wananchi wa Amerika ambao bado wana fungamano la kifamilia na kitamaduni na bara la Afrika. Wanaiona Amerika ni "kwao"; lakini Afrika pia ni "kwao". Na wale watokao Afrika Mashariki hutaka kujifunza Kiswahili kwa kuamini kwamba hii ndiyo lugha ya "kwao".

Kisha kuna like kundi la Wasomali, Wahabeshi, Waganda, na kadhalika waliowahi kuwa wakimbizi (refugees) Kenya au Tanzania kwa miaka michache. Sasa wakiwa Amerika huona wamepata fursa ya kukipalilia kile Kiswahili walichowahi kuokota hapa na pale katika maisha yao ya ukimbizi nchini Kenya au Tanzania. Na wengineo ambao asili yao si Afrika Mashariki huwa na hisia za Umajumui wa Afrika ambazo pia zinawafanya wawe na hamu ya kujifunza Kiswahili. Hisia hizi za umoja wa Afrika ambazo zinakipa Kiswahili nguvu kwa sababu ya historia yake kwa jumla na kule kukubaliwa kama lugha moja ya Umoja wa Afrika (African Union), zinatiliwa nguvu kila siku na vyama vya wanafunzi wa kiAfrika (African Students Associations), vinavyopatikana katika vyuo vingi vya Amerika. Ikiwa hisia za Umajumui wa Afrika – Umajumui wa Bara la Africa

au continental pan-Africanism, hasa – zimepungua nguvu zake barani Afrika kwenyewe, bado zinaonyesha dalili ya kuwavutia Waafrika wahamiaji wa hivi karibuni nchini Amerika.

Ilhamu hii ya kujifunza Kiswahili miongoni mwa vizazi vya wahamiaji wapya (new Diaspora), ni katika mambo ambayo yanawavutia wataalamu wa Masomo ya Uhamiaji (Migration Studies). Hii ni fani ya masomo ambayo imezidi umuhimu wake hivi karibuni kwa sababu ya idadi kubwa sana ya watu wa kila mahali duniani ambao, kwa sababu mbali mbali, wamelazimika kuondoka makwao na kuhamia kwengineko. Suala moja huulizwa mara kwa mara: Muhajirina hawa hutumia lugha gani na vipi katika mazingira yao mapya? Hudhibiti vipi lugha na tamaduni zao wakaweza kuwarithisha watoto wao? Na ikiwa wameshindwa kuzidhibiti majumbani, kuna njia gani nyingine za kuwasaidia watoto hao kujifunza lugha na tamaduni za kule watokako wazazi wao, na wanazitumia vipi katika kujitambulisha kwao katika "kwao kupya?" Maswali kama haya hayakuwa na budi kukifanya Kiswahili, katika lugha za Afrika Mashariki, kiwe miongoni mwa lugha zinazotaamaliwa ili kufahamu zaidi hali ya muhajirina nchini Amerika.

## Kihitimisho

Tukizingatia maelezo yetu mpaka sasa basi, kitu kimoja kinajitokeza waziwazi. Nacho ni umuhimu wa "vita" katika historia ya maisha na maendeleo ya Kiswahili nchini Amerika. Katika hivi ni vile Vita Baridi vya kwanza baina ya Amerika na Usovieti, Vita Baridi vya Pili baina ya Amerika na Uchina – ingawa, kama tulivyotangulia kutaja, hivi viliathiri zaidi masomo ya Kiswahili Uchina kuliko Amerika – na kulingana na maoni ya Huntington, vita vya kitamaduni baina ya Uzungu na Uislamu. Hata ile hamu ya kujifunza Kiswahili miongoni mwa vizazi vya wahamiaji wa asili ya kiAfrika – wa zamani na wa leo – pia imefungamana na dhana ya vita – vita vilivyowafanya wawe mateka au wakimbizi mpaka wakaangukia Amerika, na vita vyao vya kitamaduni dhidi ya ugozi na taasubi za Waaamerika wa asili ya Ulaya nchini Amerika. Isipokuwa katika vyuo vichache, dhana ya "amani", ya kuendeleza mafunzo ya lugha za kigeni kwa lengo la kuleta mawasiliano mema, kufahamiana na kushirikiana kwa wema, ni dhana ambayo haijakuwa na nafasi wala nguvu ya kutosha katika mipango ya serikali hasa ya kuimarisha jengo la ufundishaji wa Kiswahili na lugha nyingine nchini Amerika. Kwa mtazamo huu basi, vikisha vita baina ya Uzungu na Uislamu, pengine itabidi tutafute vita vyingine tuvianzishe ili dola ya Amerika iendelee kuyafadhili masomo ya Kiswahili katika vyuo vyake!

Lakini pia huenda masomo ya Kiswahili yakaweza kudumu Amerika ikiwa lugha yenyewe itaongezeka thamani yake barani Afrika. Bila ya shaka wananchi wa Afrika Mashariki wana jukumu kubwa katika kuhakikisha kuwa lugha hii itathaminiwa. Kama Ali Mazrui alivyowahi kusema:

> East Africa is accountable to black people everywhere for what happens to Swahili. This region is responsible for the only international language that the black world has produced. Anything short of full commitment by East Africa to further the development of Swahili would be an act of cultural abdication. Such an abdication would be unworthy of this region. (Mazrui 1975: 14)
>
> Afrika Mashariki ina wajibu mkubwa kwa watu wote weusi duniani kuhusu matokeo ya lugha ya Kiswahili. Jimbo hili lina dhima juu ya lugha ya pekee ya kimataifa inayotokana na watu weusi. Hatua yoyote isiyojizatiti kuendeleza dhima hii kikamilifu ni kulikimbia jukumu hili la kitamaduni. Na ukimbizi kama huo si lahiki ya jimbo hili.

Mpaka sasa kuna dalili nzuri kuwa thamani ya Kiswahili inaelekea kupanda Afrika. Hapana shaka kwamba tangu Kenya ilipopata uhuru Kiswahili kimepiga hatua kubwa, mpaka kukubaliwa kikatiba kuwa moja katika lugha zake rasmi. Vilevile, Kiswahili kinaendelea kupata nguvu Uganda, hasa baada ya serikali kukifanya kiwe somo muhimu katika maskuli yake. Tanzania siku zote iliongoza katika kukithamini Kiswahili. Hivi karibuni kulikuwa na wasiwasi kwamba serikali ya Tanzania inalegeza kamba kidogo katika matumizi ya Kiswahili kama lugha ya ufundishaji katika shule za msingi. Lakini wakati huohuo, Tanzania inaonyesha kuelekea kukifanya Kiswahili kama lugha ya mafundisho katika shule za sekondari.[14]

Pia tunaona maendeleo kwingineko barani Afrika. Kiswahili kilianza kufundishwa tangu zamani kidogo na kinaendelea kufundishwa katika baadhi ya vyuo kule Ghana, Nigeria, Libya na Misri. Ni kweli kwamba nguvu ya itikadi ya Umajumui wa Afrika iliyokifanya Kiswahili kianze kufundishwa katika nchi hizi tangu awali sasa imepungua sana. Na huenda udhaifu huu wa Umajumui wa Afrika umeanza kuathiri idadi ya wanafunzi wanaochagua kujifunza Kiswahili katika vyuo vya Ghana, Nigeria, na Misri. Kwa upande mwingine, siasa za kiuchumi za ujumuiya wa majimbo fulani – kama Jumuiya ya Maendeleo Kusini ya Afrika (South African Development Community, SADC) na Jumuiya ya Afrika Mashariki, Tanzania ikiwemo katika zote mbili—zimeongezeka nguvu kidogo. Kwa sababu hii, nchi kama Rwanda, Sudan Kusini, Namibia, na Afrika Kusini zote zinaonesha dalili ya kutaka kukipa Kiswahili nafasi fulani katika elimu ya watoto wao. Na hvi karibuni UNESCO imeifanya Julai 7 Siku ya Kiswahili Duniani (World Swahili Language Day), tarehe muhimu ya kuidhimisha na kuisherehekea lugha hii.

Basi mkondo huu ukiendelea Afrika Mashariki na katika nchi nyingine za Afrika, huenda tukafika wakati ambapo uhai wa masomo ya Kiswahili nchini Amerika na kwingineko duniani hautategemea tena hali ya vita, bali utakuwa na sababu mpya – sababu ya umuhimu wa lugha yenyewe kwa Waafrika wenyewe.

---

[14] See https://thisisafrica.me/african-identities/tanzania-adopts-swahili-official-language-instruction-schools/ (mara ya mwisho kufunguliwa tarehe 14-04-2023).

## Marejeleo

Attwood, William. 1967. *The Reds and the Blacks: A Personal Adventure*. New York: Harper and Row.

Berlin, Ira. 2010. The Changing Definition of African American. *Smithsonian Magazine* (February). https://www.smithsonianmag.com/history/the-changing-definition-of-african-american-4905887/ (mara ya mwisho kufunguliwa tarehe 26-03-2021).

Bundy, Colin Bundy. 2002. Continuing a Conversation: Prospects for African Studies in the 21st Century. *African Affairs* 30(2): 61-73.

French, Howard W. 2014. *China's Second Continent: How a Million Migrants Are Building a New Empire in Africa.* New York: Vintage Books.

Fukuyama, Francis. 1992. *The End of History and the Last Man.* New York: Free Press.

Gromov, Mikail D. 2018. Swahili Literature in the Russian language. *Swahili Forum* 25: 165-168.

Harries, Lyndon. 1968. The Teaching of Swahili. *The Modern Language Journal* 52(3): 146-148.

Huntington, Samuel P. 1996. *The Clash of Civilizations and the Remaking of World Order.* New York: Simon & Schuster.

Mamdani, Mahmood. 1983. *Imperialism and Fascism in Uganda.* London: Heinemann.

Markle, Seth M. 2017. *A Motorcycle on Hell Run: Tanzania, Black Power, and the Uncertain Future of Umajumui wa Afrika, 1964-1974*. East Lansing: Michigan State University.

Mazrui, Ali A. 1975. Swahili International. Is It the Only International Language That Africa Has Produced? *The Pan-Africanist* 6: 8-14.

Mazrui, Ali A. 1967. Tanzaphilia: A Diagnosis. *Transition* 31(June/July): 20-26.

Mugane, John. 2015. *The Story of Swahili.* Athens: Ohio University Press.

Paik, A. Naomi. 2013. Education and Empire, Old and New: HR 3077 and the Resurgence of the US University. *Cultural Dynamics* 25(1): 3-28.

Steger, Manfred B. 2020. *Globalization: A Very Short Introduction*, 5th Edition. New York: Oxford University Press.

Tellis, Ashley J., Alison Szawilski & Michael Wills (eds). 2020. *US-China Competition for Global Influence.* Washington D.C.: National Bureau of Asian Research.

Wilson, Amrit. 1989. *US Foreign Policy and Revolution: The Creation of Tanzania.* London: Pluto Press.